# JARIDA LA RS RUVUMA

## SEPTEMBA 2024










# TOLEO MAALUM LA ZIARA YA RAIS DKT SAMIA SULUHU HASSAN MKOANI RUVUMA

www.ruvuma.go.tz



## KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

**JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO MAALUM LA ZIARA YA RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN MKOANI RUVUMA SEPTEMBA 2024**

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

# TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wa ngazi ya Wilaya,Mkoa na kitaifa wanavyofanya ziara za kuzungumza na wananchi,kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

**RAIS SAMIA ALIVYOWASILI SONGEA KWA ZIARA YA KIKAZI**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwasili katika uwanja wa Ndege wa Songea kwa ajili ya kuanza ziara ya kikazi ya siku sita Mkoani Ruvuma kuanzia Septemba 23 hadi 29,2024.Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed.



# RAIS SAMIA AWASILI UWANJA WA MAJIMAJI KUFUNGA TAMASHA LA UTAMADUNI LA KITAIFA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

akitembelea mabanda ya Maonesho kwenye Tamasha la Tatu la Utamaduni la Kitaifa lililofanyika katika uwanja wa Majimaji mjini Songea



**RAIS SAMIA ZIARANI MKOANI RUVUMA**



RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan ameanza ziara ya kikazi ya siku sita mkoani Ruvuma kwa kufunga tamasha la utamaduni la kitaifa ambalo limefanyika kwenye uwanja wa Majimaji kuanzia Septemba 20 hadi 23 mwaka huu.



**RAIS SAMIA AWEKA SHADA LA MAUA KABURI LA MASHUJAA 66 SONGEA**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya kuweka shada la maua katika Mnara wa Mashujaa wa kaburi ambalo wamezikwa mashujaa 66 wa vita ya majimaji lililopo ndani ya Makumbusho ya

Taifa ya majimaji Songea.Rais Dkt. Samia yupo Mkoani Ruvuma kwa ziara ya kikazi ya siku sita ambapo atakagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kuzungumza na wananchi .



**RAIS SAMIA AWEKA SHADA LA MAUA KABURI LA NDUNA SONGEA MBANO**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua katika kaburi la Chifu Msaidizi wa Wangoni Nduna Songea Mbano ambaye alinyongwa na kukatwa Kichwa na Wajerumani mwaka 1906.




**NAWEZA KUCHEZA BAO PIA**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akicheza mchezo wa bao na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Dkt. Damas Ndumbaro wakati alipotembelea mabanda ya Maonesho katika uwanja wa Majimaji mjini Songea mkoani Ruvuma.Rais Samia alishinda mchezo huo.

## RAIS SAMIA AHUTUBIA WATU ZAIDI YA 50,000 UWANJA WA MAJIMAJI SONGEA




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amehitimisha Ziara yake ya Kikazi Mkoa wa Ruvuma kwa kuhutubia Maelfu ya Wananchi waliofurika Uwanja wa Majimaji Songea kwenye Mkutano wa hadhara wa kuagana na Wananchi wa Mkoa huo.

Rais Dk. Samia amesema Ziara yake mkoani humo iliyoanza Septemba 23, 2024 imekuwa na mafanikio Makubwa ambapo alitembelea Wilaya zote za Mkoa huo na kujionea namna fedha alizoleta zinatumika kutatua kero za Wananchi.

Aidha Rais Samia amewaahidi Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kuwa Serikali itaendelea kuleta fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na kusimama kikamilifu Miradi inayoendelea Sasa ikamilike kwa wakati.

## RAIS SAMIA AAGIZA BARABARA YA SONGEA - NJOMBE - MAKAMBAKO KUANZA KUJENGWA UPYA.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiagiza Wizara ya Ujenzi kukamilisha maandalizi na kuanza kujenga upya barabara ya Songea - Njombe - Makambako (km 295) pamoja na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Songea (Songea Bypass) yenye urefu wa kilometa 16 kwa kiwango cha lami.

Rais Samia ametoa agizo hilo kwa Waziri wa Ujenzi Innocent Bashungwa, wakati akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma katika mkutano wa kuhitimisha ziara yake ya kikazi uliofanyika katika Uwanja wa Majimaji Songea Mkoani humo.

"Ninafahamu barabara ya Songea - Njombe hadi Makambako sasa inahitaji matengenezo makubwa tayari nimeshaielekeza Wizara ya Ujenzi kuishughulikia pamoja na barabara ya mzunguko ya bypass ya hapa Songea hatua za kuanza kuijenga zipo mwishoni", amesema Rais Dkt. Samia.

Rais Samia ameeleza kuwa hadi kufikia mwezi Oktoba, 2024 Serikali itakuwa imempata Mkandarasi kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa barabara ya Lukuyufusi - Mkenda (km 60) kwa kiwango cha lami ili kuweza kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na nchi jirani ya Msumbiji.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia amesema kuwa tayari ameidhinisha kiasi cha Shilingi Bilioni 3.5 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa barabara ya Amani Makoro

hadi Luanda (km 35) kwa kiwango cha lami ambapo tayari Serikali imekamilisha sehemu ya barabara hiyo kilometa tano kuanzia Kitahi hadi Makolo.

Rais Dkt. Samia amewaeleza wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kuwa Serikali ina mpango wa kuunganisha Wilaya ya Nyasa na Songea Vijijini kwa kuanza ujenzi wa Daraja la Mitomoni lenye urefu wa mita 80.

Rais Dkt. Samia akiwa Mkoani Ruvuma katika ziara yake ya kikazi, Katika Sekta ya Ujenzi alikagua ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songea ambao umekamilika kwa asilimia 100 na kugharimu shilingi Bilioni 40.87 pamoja na kufungua barabara ya Mbinga - Mbamba Bay (km 66) iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na kugharimu Shilingi Bilioni 122.76



Sehemu ya barabara ya kutoka Songea hadi Makambako ambayo imechakaa na serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan inatarajia kuijengwa upya barabara hiyo

**MILIONI 38 ZILIVYOINGIZA NISHATI SAFI YA KUPIKIA SEKONDARI YA DKT.SAMIA NAMTUMBO**



.

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) imetoa sh milioni 38.2 ili kufungwa kwa mfumo wa nishati safi ya kupikia katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Dk. Samia Suluhu Hassan mkoani Ruvuma ikiwa ni utekelezaji kwa vitendo Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Shule hiyo ya kisasa yenye wanafunzi zaidi ya 540 kwa sasa ipo katika Wilaya ya Namtumbo katika Mkoa wa Ruvuma ilizinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza mara baada ya uzinduzi wa shule hiyo, Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti REA, Mhandisi Godfrey Chibulunje amemshukuru Rais kwa kuendelea kutoa fedha zinazowezesha wakala kutekeleza miradi yake mbalimbali kwa wakati ikiwamo miradi ya nishati safi ya kupikia.

“REA tunaendelea kutekeleza maelekezo ya Serikali pamoja na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa vitendo na katika shule hii tumetoa sh milioni 38.2 kwa ajili ya kufungwa mifumo ya nishati safi ya kupikia tofauti na hapo awali ambapo walikuwa wanatumia kuni kupikia,” amesema Mhandisi Chibulunje.

Mhandisi Chibulunje amesema, REA itahakikisha shule mbalimbali zinafungwa mfumo wa nishati safi wa kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na kuongeza kuwa wakala huo umesaini mikataba ya zaidi ya Sh bilioni 50 kuhakikisha taasisi zinazolisha watu zaidi ya 300 kama magereza na kambi za jeshi zinafungiwa mifumo ya nishati safi ya kupikia.

## MAHABA MAKUBWA YA WANANCHI WA RUVUMA KWA RAIS SAMIA



Maelfu ya wananchi kutoka mkoa wa Ruvuma na maeneo yake wametokelezea kwa wingi, wakiwa na hamasa na furaha tele, kumshuhudia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan, akihutubia katika mkutano mkubwa uliofanyika Uwanja wa Majimaji mjini Songea .

Mkutano huo umehitimisha ziara yake ya siku sita mkoani Ruvuma ya kukagua maendeleo na jinsi Ilani ya CCM inavyotekelezwa.



## SERIKALI KUENDELEA KUIMARISHA UPATIKANAJI WA UMEME



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini ambapo inatekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha kupokea umeme cha Tunduru ambacho utekelezaji wake umefikia asilimia 50.

Rais Samia ameyasema hayo wakati akihitimisha ziara yake mkoani Ruvuma iliyokuwa na lengo la kujipima ni kwa kiasi gani Serikali imeweza kutekeleza ahadi ilizo zitoa kwa wananchi.

Ndugu zangu kukamilika kwa mradi huu pamoja na kuunufaisha Mkoa wa Ruvuma lakini pia utapelekea kuiunganisha Mikoa ya Lindi na Mtwara kuiwezesha kupata umeme wa gridi ya Taifa." Amesema Rais Samia.

Ameongeza kuwa, Serikali inafanya juhudi kubwa katika kusogeza huduma za umeme kwenye kila kijiji ambapo Serikali kupitia REA imefikisha umeme kwenye Vijiji 541 kati ya Vijiji 551 vya Mkoa wa Ruvuma na kuongeza kuwa Serikali inaendelea kusogeza huduma kwenye vitongoji mkoani humo.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi ambao bado hawajalipwa fidia ili kupisha utekelezaji wa miradi ya umeme, kupisha utekelezaji kwani Serikali italipa fidia zao na kuongeza kuwa hakuna mwananchi ambaye hata lipwa fidia.

Pia, ametoa wito kwa viongozi wa Serikali na watumishi wa wananchi kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuokoa maisha ya watanzania pamoja na misitu.

## RAIS SAMIA ATOA TRILIONI SITA KÜTEKELEZA MIRADI CHINI YA TAMISEMI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema Serikali imetoa fedha takribani Sh. Trilioni sita tangu Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mhe. Mchengerwa ameyasema hayo wakati akitoa salamu za Wizara kwenye mkutano wa hadhara wa kuhitimisha ziara ya siku sita ya Rais Samia mkoani Ruvuma uliofanyika kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea .

Amesema "Mhe. Rais fedha ulizotoa zimeenda kila Mkoa, Halmashauri, Tarafa, Kata, Kijiji, Kitongoji na kila mtaa na zimegusa wanawake kwa wanaume, wazee, vijana, watoto na hata walemavu."

"Hakuna kundi ambalo halijafikiwa na huduma zilizopelekwa kupitia fedha hizo ulizotoa, umegusa maisha ya watanzania, umegusa mioyo yao na umeboresha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi,"amesema.


Amefafanua miradi iliyotekelezwa kwa kipindi hicho kuwa ni Hospitali za Wilaya 129 mpya zimejengwa na hospitali Kongwe 50 zimekarabatiwa, Vituo vya Afya 367 vimejengwa, majengo ya kutoa huduma za dharura (EMD) 87 yamejengwa, Majengo ya kutoa huduma za Wagonjwa mahututi 28 yamejengwa, Mitambo ya

kuzalisha hewa tiba ya Oksijeni 21 imesimikwa, magari ya kubebea wagonjwa pamoja na usimamizi wa shughuli za Afya 523 yamenunuliwa.
"Kila Halmashauri nchini imepata gari la kubebea wagonjwa pamoja na gari la usimamizi wa shughuli za afya na hapa kwenye Mkoa wa Ruvuma wamepokea magari ya Wagonjwa kwa kila Halmashauri,"amesema
Aidha, amesema kwa upande wa elimu hadi sasa Shule mpya za Sekondari kwa Kata 458 zimejengwa, Shule za Msingi 665 zenye madarasa ya awali na vyumba vya madarasa 50,050 vimejengwa pamoja na nyumba za walimu 366 zimejengwa.
"Kwa upande wa TARURA umeongeza bajeti kutoka Sh.Bilioni 253 mpaka kufikia Sh.Trilioni 1.3, ongezeko hili ni zaidi ya asilimia 300 na hii ni kwa sababu unataka kuona barabara za vijijini zikifunguliwa na wananchi wanasafirisha bidhaa zao kwa urahisi."
“ Mhe. Rais kupitia ongezeko hili umeweza kujenga barabara za lami maeneo ambao hayakudhaniwa kuwa na lami umepandisha hadhi barabara nyingi za vijijini na mijini na zaidi umeagiza tuongeze mtandao wa barabara za lami yenye urefu wa Kilometa 23 na kwa hapa Songea Manispaa tu barabara ya lami itajengwa yenye urefu wa Kilometa 12.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan akiagana na baadhi ya viongozi wa Chama na Serikali baada ya kuhitimisha ziara yake ya siku sita mkoani Ruvuma kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea

## RUVUMA IMEVUMA KWA MAENDELEO




Maelfu ya wananchi kutoka mkoa wa Ruvuma na maeneo yake wamejitokeza kwa wingi, wakiwa na hamasa na furaha tele, kumshuhudia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan, akihutubia katika mkutano mkubwa uliofanyika Uwanja wa Majimaji mjini Songea .
Mkutano huo umehitimisha ziara yake ya siku sita mkoani Ruvuma ya kukagua maendeleo na jinsi Ilani ya CCM inavyotekelezwa.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwaaga wananchi mara baada ya kumaliza mkutano wa kuhitimisha ziara yake katika uwanja wa Majimaji, Wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma tarehe 28 Septemba, 2024.

## MAMA SAMIA KARIBU TENA RUVUMA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwaaga wananchi mara baada ya kumaliza mkutano wa kuhitimisha ziara yake katika uwanja wa Majimaji, mjini Songea mkoani Ruvuma



## RAIS SAMIA NDANI YA UWANJA WA MAJIMAJI SONGEA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea tayari kwa kuhutubia wananchi wa Songea Mkoani Ruvuma.



## SERIKALI IMEJIPANGA KUINUA SEKTA YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema serikali imejipanga kuinua Sekta ya umwagiliaji kwa asilimia 50 ifikapo 2030

“Serikali imewekeza katika sekta ya umwagiliaji, na ifikapo 2030, kilimo cha umwagiliaji kinatarajiwa kufikia asilimia 50 ya kilimo nchini”, amesema Rais Samia

Samia amesema hayo wakati akihutubia wananchi katika Viwanja vya Majimaji mjini songea mkoani Ruvuma, ambapo amezungumza na wananchi kuhusu ziara yake hiyo mkoani humo, na kueleza mafanikio, mipango na maagizo mbalimbali ya serikali

Rais Samia amesema alikagua ununuzi wa mahindi katika maghala ya NFRA na kuweka jiwe la msingi kwa ujenzi wa maghala 28 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 28,000 za mazao ya nafaka, kisha alitembelea shamba la kahawa la Aviv na kusisitiza umuhimu wa kilimo cha kahawa.

Rais Samia ameongeza kuwa Serikali imetoa ruzuku ya mbolea yenye thamani ya bilioni 83.5, huku matumizi ya mbolea yakiongezeka kutoka tani 32,139 mwaka 2022 hadi tani 123,049 mwaka 2023, ambalo ni sawa na ongezeko la 283%.

Kwa upande wa zao la korosho, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 15,000 hadi tani 29,109 kwa msimu wa 2023/2024, na lengo ni kufikia tani 55,730 msimu wa 2024/2025. Serikali pia imeandaa miche bora ya kahawa milioni 20 na kuigawa kwa wakulima bure, ikilenga kuboresha masoko ya kimataifa.

“Uzalishaji wa tumbaku umeongezeka kutoka tani 250 mwaka 2021 hadi tani 4,100 msimu wa 2023/2024”, amesema Rais Samia

Rais Dkt.Samia ameongeza kuwa Mkoa wa Ruvuma una Miradi 33 ya umwagiliaji yenye thamani ya shilingi bilioni 32.4.

Kupitia NFRA, serikali imeunda mifumo ya kununua tani 170,000 za nafaka kwa thamani ya shilingi bilioni 119. Hadi sasa, tani 63,467 zimenunuliwa kwa thamani ya shilingi bilioni 44.43. Serikali itaendelea kujenga uwezo wa NFRA ili kuhakikisha usalama wa chakula nchini.



Pichani kushoto ni Katibu Mkuu wa CCM Taifa Dkt.Emanuel Nchimbi,kulia ni Waziri wa Wizara ya Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed wakiwa ndani ya uwanja wa Majimaji mjini Songea wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea.

## RAIS SAMIA AFUNGA KIKAO CHA BARAZA LA UWT TAIFA SONGEA




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akifunga Kikao Maalum cha Baraza Kuu la Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) Taifa katika ukumbi wa Parokia ya Bombambili, Wilaya Songea Mkoani Ruvuma,



## RAIS SAMIA KATIKA SEKONDARI YA WASICHANA YA DKT SAMIA NAMTUMBO



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mchepuo wa Sayansi na Sanaa ya Dkt.. Samia Suluhu Hassan iliyopo katika kitongoji cha Migeregere kata ya Rwinga, Wilaya ya Namtumbo, Mkoani Ruvuma



## SEKONDARI YA DKT SAMIA NAMTUMBO MIONGONI MWA SEKONDARI 26 BORA NCHINI



Sekondari ya Dkt Samia Suluhu Hassan ya Namtumbo mkoani Ruvuma ni miongoni mwa shule 26 za Wasichana za Sayansi za Mikoa zilizojengwa kwenye Mikoa yote Tanzania bara na imejengwa kwa gharama ya shilingi Bil. 4.6 ikiwa na vyumba vya madarasa 22, mabweni 8, nyumba za walimu 3 (2 in 1), Nyumba ya Mkuu wa shule, Nyumba ya Matron, chumba cha TEHAMA, Maktaba, Jengo la Utawala pamoja na uzio upande wa Mabweni.

Shule hii ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 na mpaka sasa wanafunzi waliopo ni 548.



## RAIS SAMIA AZINDUA SEKONDARI YA WASICHANA YA DKT.SAMIA NAMTUMBO



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mchepuo wa Sayansi na Sanaa ya Dkt.. Samia Suluhu Hassan iliyopo katika kitongoji cha Migeregere kata ya Rwinga, Wilaya ya Namtumbo, Mkoani Ruvuma.

Shule hii ni miongoni mwa shule 26 za Wasichana za Sayansi za Mikoa zilizojengwa kwenye Mikoa yote Tanzania bara na imejengwa kwa gharama ya shilingi Bil. 4.6 ikiwa vyumba vya madarasa 22, mabweni 8, nyumba za walimu 3 (2 in 1), Nyumba ya Mkuu wa shule, Nyumba ya Matron, chumba cha TEHAMA, Maktaba, Jengo la Utawala pamoja na uzio upande wa Mabweni.

Shule hii ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 na mpaka sasa wanafunzi waliopo ni 548.

Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanamshukuru sana Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea shule hiyo maalum ya wasichana ambayo ni mkombozi wa Watoto wa kike wa Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla.

## RAIS SAMIA AKIZUNGUMZA NA WANAFUNZI WA SEKONDARI YA DKT.SAMIA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na wanafunzi, wazazi na wananchi mara baada ya kuzindua Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mchepuo wa Sayansi na Sanaa ya Dkta. Samia Suluhu Hassan iliyopo katika kitongoji cha Migeregere kata ya Rwinga, Wilaya ya Namtumbo, Mkoani Ruvuma.



# RAIS SAMIA NA WANAFUNZI WA SEKONDARI YA DKT.SAMIA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mchepuo wa Sayansi na Sanaa ya Dkt.. Samia Suluhu Hassan iliyopo katika kitongoji cha Migeregere kata ya Rwinga, Wilaya ya Namtumbo, Mkoani Ruvuma.



**MATUKIO KWENYE UZINDUZI WA SEKONDARI YA DKT.SAMIA NAMTUMBO**




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mchepuo wa Sayansi na Sanaa ya Dkt.. Samia Suluhu Hassan iliyopo katika kitongoji cha Migeregere kata ya Rwinga, Wilaya ya Namtumbo, Mkoani Ruvuma .



# RAIS SAMIA ALIVYOSOMEWA DUA TUNDURU



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akishukuru mara baada ya kusomewa Dua katika Msikiti Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Mkoani Ruvuma



# HABARI PICHA ZIARA YA RAIS WILAYANI TUNDURU




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa (kulia) katika mkutano wa hadhara uwanja wa CCM wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma Katikati ni Mkuu wa Mkoa Ruvuma , Kanali, Ahmed Abbas Ahmed



Wananchi wa Tunduru wakiwa kwenye mkutano wa hadhara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan uliofanyika katika Uwanja wa CCM Tunduma Mkoani Ruvuma.

## RAIS SAMIA AZINDUA SOKO LA MADINI YA VITO TUNDURU




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan baada ya kuzindua soko la madini ya vito Tunduru mkoani Ruvuma



## MKUTANO WA HADHARA WA  RAIS SAMIA TUNDURU



Wananchi wa Tunduru wakiwa kwenye mkutano wa hadhara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan uliofanyika katika Uwanja wa CCM Tunduma Mkoani Ruvuma.



**RAIS SAMIA AKIZUNGUMZA NA WANANCHI WA TUNDURU**




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia wananchi katika uwanja wa CCM wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.



HAKUNA MGONJWA ANAYEBEBWA KWENYE TENGA TUNDURU' MHE. MCHENGERWA

# HAKUNA MGONJWA ANAYEBEBWA KWENYE TENGA TUNDURU



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema hakuna mgonjwa anayesafirishwa kwa njia ya Pikipiki huku akiwa amewekwa kwenye tenga kupelekwa kupata huduma za afya katika Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma

Mhe. Mchengerwa ameyasema hayo wakati akitoa salamu za Wizara kwenye mkutano wa hadhara wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na wananchi wa Tunduru uliofanyika kwenye uwanja wa Ccm mjini Tunduru.

Amesema ameona taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zikionesha mgonjwa akisafirishwa kwenye Pikipiki huku akiwa kwenye tenga na kueleza kuwa hakuna magari ya kusafirishia wagonjwa jambo ambalo ni upotashaji.

"Napenda kukuthibitishia Mhe. Rais hapa Tunduru hakuna upungufu wa magari ya kubebea wagonjwa na kati ya Magari 535 tuliyoyakabidhi mwaka jana kwa muongozo wako Mhe. Rais hapa Tunduru walipata Magari mapya manne ya kubebea wagonjwa"'alisisitiza

Amesema magari hayo yalipekwa kwenye Kituo cha Afya Nakapanya, Matemanga, Nalasi na Mchesi ambayo yanafanya kazi saa 24 na rufaa zote zinaratibiwa kwa utaratibu maalumu na sio kuchangisha wananchi.

Ameutaja utaratibu unaotumika kusafirisha wagonjwa ni kutumia magari ya kubebea wagonjwa na kwa kutumia madereva ngazi ya jamii waliosajiliwa wakati wa mfumo wa M-Mama ambapo mfumo huu unahusika na kusafirisha wakina mama wajawazito na watoto wachanga bila malipo yoyote.

Ameongeza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina jumla ya madereva wa jamii 20 walioingia mikataba na Serikali; Hivyo taarifa hizi zipuuzwe kwani zinalengo la kuupotosha umma, kuleta taharuki kwa jamii na kuichafua Serikali.


## HABARI PICHA ZIARA YA RAIS SAMIA KIJIJI CHA LITOLA NAMTUMBO



Maelfu ya Wananchi wa Kata ya Litola Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma waliofurika Barabarani kumlaki Rais Dkt samia Suluhu Hassan wakati wa Ziara yake Mkoani Ruvuma



## MUONEKANO WA BARABARA YA MBINGA-MBAMBABAY



Mwonekano wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay Mkoani Ruvuma yenye urefu wa kilometa 66 iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na kufunguliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Zaidi ya shilingi bilioni 122 zimetekeleza mradi huu na kuufungua ushoroba wa Mtwara unaopitia Mkoa wa Ruvuma



## HABARI PICHA RAIS SAMIA KATIKA KIJIJI CHA RWINGA NAMTUMBO



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwasalimia wananchi wa Kata ya Rwinga, Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma



**RAIS SAMIA AISHUKURU BENKI YA MAENDELEO AFRIKA KWA UWEZESHAJI KWENYE MIUNDOMBINU TANZANIA**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameishukuru na kuipongeza Taasisi ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kuwa mdau mkubwa wa sekta ya miundombinu nchini ambapo wamewezesha mkopo wa Shilingi Bilioni 630 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) kwa kiwango cha lami na barabara nyingine.

Dkt. Samia ametoa pongezi hizo wakati akizungumza na wananchi Wilayani Nyasa mara baada ya kufungua barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 16) iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi Bilioni 122.76 Mkoani Ruvuma.

“Nataka niwaambie benki ya AfDB hawajasaidia barabara hii peke yake, ni wadau wetu wa barabara nchi nzima na hivi tunavyozungumza wanatusaidia kujenga barabara ya mzunguko ya njia nne katika mji Mkuu wa Dodoma”, Amekaririwa Dkt. Samia.

Dkt. Samia ameeleza kuwa kukamilika kwa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) kwa kiwango cha lami utasaidia kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa abiria na bidhaa na amewataka wananchi kutumia uwepo wa barabara hiyo kuleta maendeleo katika Wilaya ya Nyasa na Mkoa wa Ruvuma kiujumla.

Aidha, Dkt. Samia ametoa wito kwa watumiaji wa barabara hiyo hususani madereva kuwa waangalifu ili barabara iweze kudumu kwa muda mrefu zaidi.

Kwa upande wake, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ameishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kuendelea kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ambapo wamekamilisha kujenga kwa kiwango cha lami mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 2,384 ambayo ni sawa na asilimia

20 ya mtandao wote wa barabara unaosimamiwa na Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS).

Kadhalika, Bashungwa ameeleza kuwa Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS ipo katika hatua za kutafuta Wakandarasi kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa ujenzi wa madaraja mawili ambayo ni Daraja la Mkili lenye urefu wa mita 20 pamoja na Daraja la Mitomoni lenye urefu wa mita 80 ambalo litaunganisha Wilaya ya Nyasa na Songea Vijijini.

Kwa upande wake, Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Patricia Laverley, ameleeza utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya urafiki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki hiyo na kusema kuwa kukamilika kwa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay kutasaidia kupunguza muda wa safari, nauli pamoja na gharama za matengenezo.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Mohamed Besta ameeleza kuwa Barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) imefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika chini ya mradi wa “Transport Sector Support Programme” (TSSP) na kutekelezwa na Mkandarasi China Henan International Cooperation Group kutoka China na Mhandisi Mshauri kutoka SMEC International Pty kutoka Australia kwa gharama ya Shilingi Bilioni 122.76



Sehemu ya barabara ya lami  nzito kutoka Mbinga hadi Mbambabay wilayani Nyasa mkoani  Ruvuma yenye urefu wa kilometa 66 ambay serikali imetumia Zaidi ya shilingi bilioni 122 kutekeleza mradi huo uliozinduliwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan

# RAIS SAMIA AFUNGUA BARABARA YA MBINGA-,MBAMBABAY




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akifungua Barabara mpya ya kiwango cha lami ya Mbinga – Mbamba Bay yenye urefu wa kilomita 66 katika Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma



# RAIS SAMIA AWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI BANDARI YA MBAMBABAY




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiweka Jiwe la Msingi la ujenzi wa bandari mpya ya Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa mkoani Ruvuma



# RAIS SAMIA ARIDHISHWA NA JENGO JIPYA LA HALMASHAURI YA MBINGA



Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dk.Samia Suluhu Hassan ameridhishwa na ujenzi wa Jengo la kisasa la ghorofa moja la Halmashauri ya wilaya ya Mbinga ambalo limejengwa kwa shilingi bilioni 3.3 hadi kukamilika kwake.

Alisema kuwa anawashukuru amefika Mbinga kwa madhumuni ya kufungua jengo na amewapongeza halmashauri hiyo kwa kukamilisha ujenzi huu wa jengo hilo zuri.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan hayo ameyasema wakati akifungua jengo la ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga mkoani Ruvuma.

Akizundua jengo hilo Septemba 25/2025 amesema kukamilika kwa jengo hilo ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) baada ya kukamilika jengo hilo wahakikishie huduma zote zinatolewa ndani ya nyumba moja .

“Ni jengo zuri nimeingia ndani kuangalia ujenzi unaridhisha sana na ni jengo lenye nafasi za kutosha kwa hiyo nawashukuru sana lakini pamoja na hilo niwapongeze madiwani kwamba mmesimamia ujenzi wa jengo hili lakini pia mmewaza kuwa na jengo la kitega uchumi jengo la kuwawezesha wananchi nimuombe Mungu awatie nguvu na mlimalize jengo hilo liweze kufanya kazi iliyokusudiwa” alisema Rais Samia.

Alisema kuwa kukamilika kwa jengo hilo ni kukuwa kwa utawala bora kwa kwamba maofisa wote wakiwemo wakuu wa Idara na kila mtu yumo humo ndani kwa maana hiyo huduma zote zitatolewa ndani ya nyumba moja ili kuharakisha huduma kwa wananchi.

” Niwasisitize watakaotumia nyumba hii madhumuni ya serikali kujenga nyumba hizi ni kuleta mazingira mazuri kwa maafisa wetu wanaofanya kazi ndani ya

halmashauri hizi ni kurahisisha utendaji wa kazi kwa hiyo niwaombe sana maofisa wote kutumia Majengo haya kwa kutulia na kufanya kazi zao vizuri kwa kuhudumia wanachi kwa upendo na weledi zaidi.”alisema Rais Samia.

Naye Mbunge wa jimbo la Mbinga Vijijini Mheshimiwa Benaya Kapinga amesema,Wanamshukuru Rais kwa miradi mingi aliyoipeleka kwenye jimbo hilo wamepata miradi ya maji bilioni 13.9 , barabara-Amani Makolo-Ruanda bilioni 60 ‘



Muonekano wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga lililozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.



**RAIS SAMIA ALIVYOZINDUA JENGO LA HALMASHAURI YA MBINGA**




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbinga mkoani Ruvuma ambapo serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 3.5 kutekeleza mradi huo uliokamilika kwa asilimia 100



**RAIS SAMIA KATIKA JIMBO LA PERAMIHO**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Wananchi wa Jimbo la Peramiho, katika muendelezo wa Ziara yake ya Kikazi mkoani Ruvuma



**RAIS SAMIA KATIKA SHULE YA CHIFU ZULU SONGEA**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewapongeza Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa kutenga fedha za mapato ya ndani zaidi ya Sh.Milioni 600 na kujenga Shule ya Msingi ya mchepuo wa Kingereza ya Chief Zulu.

Mhe. Rais ametoa pongezi hizo wakati akizungumza na wazazi na wanafunzi baada ya kuzindua shule hiyo Manispaa ya Songea.

"Nawapongeza sana Manispaa ya Songea kwa kutenga fedha zaidi ya shilingi milioni 600 kutoka kwenye mapato yenu ya ndani na kuamua kujenga shule hii muhimu kwa taaluma ya watoto wa Mkoa wa Ruvuma; Nimefarijika kuona mmejenga kuanzia madarasa ya awali ambayo yanawasaidia watoto kwenye malezi na makuzi bora kabla hawajaanza darasa la kwanza,"amesema.

Aidha ameziagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI kutafuta walimu wabobevu wa kufundisha Lugha ya Kingereza ili watoto hao waijue lugha hiyo kwa ufasaha.

"Shule kama hizi zinazofundisha Kingereza mnatakiwa kuweka walimu wanaoijua lugha hii vizuri ili kuwanoa watoto hawa kuwa mahiri kwenye lugha ya Kiingereza na sio kingereza cha kubabaisha,"amesema.

Aidha Mhe. Rais amesema kuwa serikali itaendelea kuboresha Sera ya Elimu ili kuendana na mabadiliko ya Dunia hivyo kwa sasa.

"Manavyoendelea kuongeza shule za michepuo ya Kingereza msisahau lugha yetu ya Kiswahili lakini pia mkaangalia lugha nyingine tunayoweza kuwafundisha watoto wetu ambayo ni fursa huko Duniani kama Kichina, Kifaransa nk…Katika hili mnaweza kugawa Mikoa kwa Kanda hivyo Mikoa kadhaa ikawa na shule za kufundisha Kingereza na lugha nyingine muhimu ya Kimataifa na shule za Mikoa

mingine nazo zikafundisha Kiingereza na somo lingine ili tuweze kuwa na wataalam wengi wa lugha wanaoweza kupata soko kimataifa,"amesema.
Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema hadi sasa nchini shule hizo za Mchepuo wa Kingereza ziko 68 ambazo zinafundisha lugha ya Kingereza.
Shule ya Chifu Zulu ina wanafunzi wa awali na Msingi 491 na wanafundishwa masomo yote kwa lugha ya kingereza isipokuwa kwa somo la Kiswahili.

## WANAFUNZI SHULE YA CHIFU ZULU WALIVYOMSHANGAZA RAIS SONGEA



Mwanafunzi mmoja wa Shule ya Awali na Msingi ya Mchepuo wa Kingereza ya Chief Zulu iliyopo Manispaa ya songea alijitokeza na kumzawadia Rais shillingi 50 na kupelekea wanafunzi wengine kumzawadia pia, Kwa Jumla Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepokea shilingi 1800 kutoka kwa wanafunzi hao,



Wanafunzi wa shule ya msingi ya Chifu Zulu iliyopo Manispaa ya Songea walimshangaza Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan baada ya kumchangia fedha



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Watawa wa Shirika la Benedicto wa Tutzing mara baada ya kutembelea Kanisa la Mt. Benedicto, Parokia ya Peramiho, Jimbo Kuu la Songea mkoani Ruvuma

**RAIS SAMIA  KATIKA HALMASHAURI YA MADABA**




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akivuta kitambaa kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa Ghala la nafaka Luhimba Halmashauri ya Madaba wilayani Songea kwa niaba ya maghala ya kuhifadhia nafaka yanayojengwa mkoani Ruvuma wakati wa muendelezo wa ziara yake Mkoani Ruvuma



Moja ya maghala yaliyozinduliwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan Madaba

## RAIS SAMIA KATIKA SHAMBA LA KAHAWA LA AVIV SONGEA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akichambua Kahawa wakati alipotembelea Shamba la Kahawa la Aviv Tanzania Limited lililopo Mkoani Ruvuma

## RAIS SAMIA NA WATOTO WA ABASIA YA PERAMIHO



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na Watawa wa Shirika la Benedicto wa Tutzing mara baada ya kutembelea Kanisa la Mt. Benedicto, Parokia ya Peramiho, Jimbo Kuu la Songea mkoani Ruvuma



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

akiwa kwenye picha ya pamoja na Wanafunzi na Walimu wa Shule ya Awali na Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Chief Zulu, iliyopo Manispaa ya Songea mkoani
Ruvuma



Picha ya chini ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mwanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Chief Zulu Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma Teofilo Mbunda kuhusu matumizi ya kompyuta shuleni hapo.
Rais Samia yupo mkoani Ruvuma kwa ziara ya kikazi



# RAIS SAMIA KATIKA MRADI WA MAJI MTYANGIMBOLE MADABA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la Msingi la mradi wa maji wa Mtyangimbole, Madaba mkoani Ruvuma,mradi huo umegharimu shilingi bilioni 5.5



# RAIS SAMIA ATEMBELEA MAKUMBUSHO YA TAIFA YA MAJIMAJI SONGEA




RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan akiwa ndani ya Makumbusho ya Taifa ya Majimaji mjini Songea .
Hii ndiyo Makumbusho pekee nchini ambayo unaweza kuona vifaa halisi vilivyotumika na babu zetu katika harakati za ukombozi dhidi ya wakoloni zaidi ya miaka 119 iliyopita



## RAIS SAMIA NDANI YA MAKUMBUSHO YA MAJIMAJI





RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu alipotembelea Makumbusho ya Taifa ya majimaji yaliyopo Mahenge  mjini Songea



## MAKUMBUSHO YA TAIFA YA MAJIMAJI YEMESHEHENI HISTORIA YA HARAKATI ZA UKOMBOZI WA MTANZANIA



RAIS Samia Suluhu Hassan ametembelea Makumbusho ya Vita ya Maji Maji yaliyopo Mahenge Songea mkoani Ruvuma kwa lengo la kutoa heshima ya kumbukizi ya mashujaa wa vita ya Majimaji vilivyoanza mwaka 1905-1907.
Mashujaa 67 waliuawa kikatili na wajerumani kwa kunyongwa mwaka 1906 na kuzikwa katika makaburi mawili yaliyopo ndani ya makumbusho ya Majimaji .



**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**
**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**


**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**

**SIMU Nambari. 025-2602256/2602238**

**FAX Na. 2602144**

**E -MAIL:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz**

**TOVUTI: www.ruvuma.go.tz**

**INSTAGRAM: rs ruvuma**

**FACEBOOK: rs ruvuma**

**YOUTUBE: rs ruvuma**